

O F I S I Y A R A I S I - T A M I S E M I
H A L M A S H A U R I Y A W I L A Y A Y A M W A N G A

**SHULE YA SEKONDARI YA KUTWA NDORWE,
S.L.P 280,
USANGI,
21/12/2020.**

Kumb Na: NSS/VOL1/2021/1

MZAZI/ MLEZI WA

S.L.P

USANGI.

**Yah: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NDORWE ILIYOKO
WILAYA YA MWANGA MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021**

1.0 Utangulizi

Ninafuraha kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Ndorwe Sekondari.

Shule ya Sekondari Ndorwe ipo katika kata ya Chomvu Tarafa ya Usangi umbali wa **km 26** kutoka makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga.

Muhula wa kuanza masomo utaanza tarehe **11/01/2021** lakini kidato cha kwanza watapokelewa shuleni tarehe **12/01/2021**. Mzazi hakikisha unamleta mwanao shuleni siku hiyo bila kukosa tarehe ya mwisho ya kuripoti kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza ni tarehe **29/01/2021**.

2.1 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za shule

- a. Sare ya shule hii ni Suruali ya kijani na shati jeupe la mikono mifupi kwa Wavulana na sketi rangi ya kijani na shati jeupe mikono mifupi kwa Wasichana

Maelezo ya Mashono: i) *WAVULANA*:- Suruali pana na iwe na marinda mawili na iwe na turn-up (Upinde wa chini Miguuni),
ii) *WASICHANA*:- Sketi ndefu inayovuka Goti na iwe na marinda.

- b. Kwa wale wasichana wanaopenda kushona Hijabu wanaruhusiwa.
- c. Viatu vyeusi na soksi nyeupe kwa wasichana na Wavulana viatu vyeusi na soksi nyeusi na mkanda mweusi wa suruali.
- d. Sweta la kijani kwa Wavulana na Wasichana.

N.B.

Mzazi/Mlezi anapaswa kumuandalia mwanae sare za shule kama zilivytajwa hapo juu. Anapokuja shuleni awe amevaa sare ya shule ulioelekezwa umuandalie